

CHUKUA TAHADHARI DHIDI YA NJAMA ZA RIBA !

السؤال: هناك بنك يشتري كل ما أطلب به من أثاث أو قطعة أرض أو سيارة بشرط : أن أكون موظف ، وأن أحول راتبي في ذلك البنك ولمدة خمس سنوات ، وذلك ضماناً لحقه ، فمثلاً : أذهب إلى ذلك البنك وأقول له : أريد منك شراء سيارة ، فيقول لي : اذهب إلى الشركة أو المعرض الذي توجد فيها السيارة التي تريدها ، وأعطي من ذلك المعرض أو تلك الشركة ورقة رسمية مبين فيها قيمة السيارة ، فإذا أحضرت الورقة ، أعطاني شيك باسم تلك الشركة أو المعرض به قيمة السيارة ، وبرفقته ورقة مكتوبًا فيها : ادفعوا حامل هذا الشيك سيارته ، فإذا كان ثمن السيارة مائة ألف ريال ، فإنه يُضيّف عليها 7 % للسنة الواحدة مقابل البيع الأجل ، ولمدة خمس سنوات ، فيصبح ثمن السيارة على في الأوراق الرسمية لدى البنك مائة وخمس وثلاثون ألف ريال . وهناك مثال آخر : إذا أردت شراء قطعة أرض فإنه يتطلب مني إحضار ورقة من مكتب العقار أين فيها قيمة الأرض ، ثم يدفع إلى الشيك وينصيّف 7 % فائدة مقابل الأجل ولمدة خمس سنوات ، فإذا كان ثمن الأرض مائة ألف ريال يصبح على لذلك البنك 135 ألف ريال ، هل هذا البيع نوع من أنواع بيع السلم ، لأنه ضمن حقه مقدماً ، ولمدة خمس سنوات ، حيث أني موظف ، وأخذ علىي أوراق وتعهدات بموجبها تحول راتبي لصالح ذلك البنك ، فيأخذ كل شهر قسطه ، ويترك لي الباقى ، وهل هذا البيع جائز شرعاً أم لا ؟ .

الجواب: لا يجوز التعامل بالمعاملة المذكورة ، لأنّ حقيقتها قرض بزيادة مشروطة عند الوفاء ، والصورة المذكورة مجرّد حيلة ، وإلا فهي معاملة ربوية محرمّة في الكتاب والسنة وإجماع الأمة ، فيجب ترك التعامل بها طاعة الله ولرسوله ﷺ : { وَمَنْ يَتَّقَ اللهُ يَجْعَلُ لَهُ مُخْرَجًا وَيَرْزُقُهُ مِنْ حِلْيَةٍ }

يختسب .

SWALI

Kuna benki ambayo inanunua kila ninachokihitaji kama vile samani za ndani au kiwanja au gari , kwa sharti : Niwe mfanyakazi , na mshahara wangu upitie katika benki hiyo kwa muda wa miaka mitano ili benki ichukue dhamana ya haki yake . Mfano nikienda katika benki hiyo na nikasema ninahitaji mninunulie gari , wataniambia , nenda katika kampuni ya uuzaaji wa magari au katika maeneo yauzayo magari ambapo kuna gari unalolitaka na utuletee

العنوان: فتاوى المسئلة الدائمة لل沐麻提
العنوان: فتاوى المسئلة الدائمة لل沐麻提

kutoka huko kwenye kampuni hiyo au sehemu hiyo , utuletee karatasi rasmi inayooonesha kiwango cha thamani ya gari . Pindi ninapoifikisha karatasi hiyo benki watanipa hundi (cheque) ambayo imeandikwa jina la hiyo kampuni au sehemu iuzayo gari , ndani ya hundi hiyo kuna kiwango cha thamani ya gari hilo na sambamba na hundi hiyo kuna karatasi nyingine (wananipa) ambayo imeandikwa "mpeni gari yake mwenye hundi hii " Endapo thamani ya gari ni Riali laki moja , basi huongezwa asilimia saba (7%) juu ya deni langu kila mwaka kwa niaba ya ulipaji wa kidogokidogo ; hivyo kwa kipindi cha miaka mitano inakuwa thamani ya gari (nitakiwayo kuilipa) ilioandikwa kwenye karatasi ya deni la benki ni Riali laki moja na elfu thelathini na tano .

Na kuna mfano mwagine ufuatao: ninapotaka kununua kiwanja , benki itanihitajia ni-wapelekee karatasi kutoka katika ofisi za ardhi yeny kubainisha ndani yake thamani (bei) ya kiwanja hicho , kisha benki itanipatia hundi (cheki) , na benki itaongeza asilimia saba (7%) juu ya bei ya kiwanja hicho kwa sababu ya ulipaji wa kidogokidogo kwa muda wa miaka mitano . Endapo bei ya kiwanja ni Riali laki moja , basi deni langu ninalodaiwa na benki litakuwa Riali laki moja na elfu thelathini na tano . Je biashara hii ni mojawapo ya aina za biashara za ulipaji wa kuchelewesha unaoruhusiwa kisheria ? Kwa sababu benki imetangulia kuchukua dhamana yake -kwa kuwa mimi ni mfanyakazi- benki ikachukua dhamana ya kuandikisha makubaliano ambayo yatapelekea kuhamishwa mshahara wangu wa mwezi moja kwa moja kuelekea katika benki hiyo , wao huchukua fungu lao na wananiachia kilichobaki , (hili hufanyika) ndani ya muda wa miaka mitano . Na je biashara hii inafaa kisheria?

JAWABU:

Haifa kufanya muamala huo uliotajwa , kwa sababu uhalsia wake ni kama mkopo unaoambatana na ziada (ya malipo) , ziada ambayo imewekewa sharti wakati wa kuplica deni (uzidishe kiwango maalumu 7%). Na hiyo sura iliyotajwa ni ujanja na njama tu (za kukwepa riba) , lakini uhalsia ni muamala wa riba ulioharamishwa ndani ya Qur'an na Sunna na Makubaliano ya wanachuoni . Ni wajibu kuacha kufanya muamala huo kwa ajili ya kumtii Allah na Mtume wake ﷺ ; na Allah anasema ((Na ambaye anamcha Allah , Allah atamjaalia mapito na atamruzuku kwa namna asiyotarajia)) .

وصلى الله على محمد وعلى آله وصحبه وسلم